



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA

Kumb. Na..KGR/MLB/MFG/099

Tarehe:17/02/2021

YAH: TANGAZO LA KARANTINI YA UGONJWA WA HOMA YA NGURUWE

Kwa mamlaka niliyopewa na **Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na.17** ya mwaka 2003, sehemu ya tatu kifungu cha 16 na sehemu ya tano kifungu cha 34, Mimi Dkt. Emmanuel Balilemwa Kaijage, Daktari wa Mifugo, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, natangaza uwepo wa Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe katika kata za **Mushabago, Kabirizi** na **Nyakatanga**.

Dalili kuu za ugonjwa huu ni nguruwe kukosa hamu ya kula, homa kali, mwili kutetemeka, miguu kukosa nguvu, mabaka mekundu kwenye ngozi yenye kuvia damu na vifo vya ghafla.

Kwakuwa ugonjwa huu unaenea kwa kasi kupitia uchinjaji na usafirishaji wa nguruwe, natangaza kuwa eneo lote la **Halmashauri ya Wilaya ya Muleba** limewekwa chini ya **Karantini** kuanzia **17/02/2021** hadi hapo itakapo tangazwa vinginevyo

Katika kipindi chote cha karantini yafuatayo nilazima yazingatiwe ili kuhakikisha ugonjwa huu unadhibitiwa.

- Uchinjaji wa nguruwe na uuzaji wa nyama (kitimoto) umesitishwa kwa muda wote wa karantini, hivyo maeneo yote yanayochinja nguruwe na yanayofanya biashara ya kuuza nyama (kitimoto) yamefungwa na hakuna ruhusa kwa mtu yeyote anayeruhusiwa kuchinja nguruwe au kuuza nyama.
- Hakuna ruhusa kwa mtu yeyote kutoa au kuingiza, kusafirisha nguruwe au mazao yote yatokanayo na nguruwe katika eneo hili isipokuwa kwa **idhini ya maandishi ya Daktari wa Mifugo (W)**